TANGAZO LA SERIKALI NA. 921 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USAFI, AFYA NA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"biashara" maana yake ni aina yoyote ya shughuli halali ya kiuchumi inayomuingizia mtu kipato;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa au sumu;

"choo bora" maana yake ni choo chenye shimo lililojengwa madhubuti kwa sakafu, na kujengewa banda lililoezekwa lenye milango na mifumo

imara inayosafirisha uchafu kwenda kwenye shimo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Arusha;

"huduma" maana yake ni huduma inayotolewa chini ya Sheria Ndogo hii;

"jengo" maana yake ni nyumba, hema, kibanda, kontena na aina yoyote ya muundo wa jengo linalotumika au lisilotumika lililopo ndani ya eneo la Halmashauri;

"kaya" maana yake ni familia yenye baba, mama na watoto au mtu yeyote aliyefikia umri wa miaka kumi na nane awe na mtoto au bila mtoto;

"kero" maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa kwa mtu kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha afya ya binadamu pamoja na viumbe wengine;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kituo cha taka" maana yake ni kituo kilichowekwa kwa madhumuni ya jamii inayoishi au inayofanya kazi, biashara jirani na kituo hicho kuweka taka ngumu kabla ya kusafirisha hadi kwenye dampo rasmi la taka ngumu;

"kizimba" maana yake ni kituo kilichojengwa maalimu kwa ajili ya kukusanyia au kuhifadhia taka kwa muda ili zisafirishwe kutupwa kwenye dampo;

"mabwawa ya maji taka" maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji taka;

"maji taka" maana yake ni maji machafu yanayozalishwa kutokana na shughuli za majumbani au viwandani;

"mazalia ya wadudu" maana yake ni sehemu ambayo wadudu hufanya mazalia au kuishi kwa minajilia ya kufanya mzunguko wa maisha;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku,

na wanyama wengine wafugwao na binafsi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha;

"mtandao wa maji taka" maana yake ni mfumo wa bomba kuu lililojengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha maji taka toka kwenye Mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye Mabwawa ya maji taka;

"pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu;

"taka za bustani" maana yake ni taka zinazotokana na shughuli za kuandaa, kulima, kutengeneza au kupalilia bustani;

"taka hatarishi" maana yake ni taka zozote zinazoweza kusababisha madhara ya kiafya kwa binadamu na viumbe hai wengine katika mazingira;

"taka za nyumbani" maana yake ni taka zote zinazozalishwa kutokana na shughuli za kila siku za nyumbani;

"taka ngumu" maana yake ni taka zote zisizo katika mfumo kimiminika;

"taka za viwandani" maana yake ni taka zote zilizo katika mfumo yabisi, kimiminika au gesi zitokanazo na shughuli za viwandani;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ukaguzi wa mazingira

4. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuingia na kukagua nyumba, kiwanja, barabara, njia, uchochoro, mfereji au ardhi na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kutunza mazingira

5.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu au laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Ni wajibu wa mtu yeyote anayeishi, anayetoa huduma, anayepata huduma au anayepita katika eneo lolote ndani ya Halmashauri kutunza mazingira.

(3) Ni wajibu wa mtu yeyote anayeishi au kutoa huduma ndani ya Halmashauri kuzingatia miongozo, kanuni na taratibu za kiafya zilizoweka au zitakazowekwa na Halmashauri.

Wajibu wa kujenga na kutumia choo bora

6.-(1) Ni wajibu wa kila mtu mwenye mamlaka ya usimamizi wa jengo linalotumiwa na mtu au watu ndani ya Halmashauri kuhakikisha kwamba kunakuwa na choo bora.

(2) Ni wajibu wa kila mtu ndani ya Halmashauri kuhakikisha kuwa anatumia choo.

Choo sehemu ya kazi

7. Kila mmiliki au msimamizi wa jengo lolote lonalotumika kwa biashara atapaswa kujenga choo katika jengo hilo.

Choo cha watu wenye mahitaji maalumu

8. Mtu yeyote anaetaka kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalumu atatakiwa kuzingatia masharti atakayopewa na Halmashauri.

Choo cha muda

9.-(1) Mtu yeyote anayetaka kujenga au kuweka choo cha muda sehemu ya ujenzi, sherehe, kambi au sehemu yoyote ambayo inakutanisha watu kwa muda ni lazima ajenge au aweke choo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

(2) Choo cha muda kitahamishwa au kuvunjwa na kufukiwa baada ya kazi au kusudio kumalizika.

Umbali wa kujenga choo kutoka kwenye chanzo cha maji.

10. Mtu yeyote atatakiwa kujenga choo umbali wa zaidi ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji.

Wajibu wa kutupa taka katika maeneo maalumu

11.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kukusanya na kusafirisha taka kutoka majumbani, kwenye vituo vya taka au vizimba hadi kwenye dampo kwa ratiba ambayo kila mtu atalazimika kuifuata.

(2) Kila mtu ana wajibu wa kutupa taka katika kituo cha taka au kizimba.

(3) Kila kaya inapaswa kuwa na chombo maalumu chenye mfuniko kitakachotumika kutupia taka ngumu na kuzimwaga katika kituo cha taka au kizimba au kwenye gari la taka kadiri ya ratiba ilivyo katika kata, kijiji au kitongoji.

(4) Mtu yeyote anayezalisha taka hatarishi atalazimika kuzitupa au kuteketeza kwa kuzingatia taratibu za utupaji wa taka hatarishi.

Ushuru wa taka ngumu

12.-(1) Mtu yeyote atawajibika kulipa ushuru wa taka ngumu kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza na la Pili.

(2) Halmashauri inaweza kuteua wakala wa kukusanya ushuru wa taka.

(3) Ushuru wa taka utalipwa kila mwezi na mwisho wa kulipa utakuwa tarehe tano ya kila mwezi unaofuata.

(4) Mtu yeyote anayezalisha taka nyingi zinazoilazimu Halmashauri au wakala kuzoa kwa ratiba tofauti na ratiba iliyowekwa atalazimika kulipa gharama za kuzoa na kusafirisha taka hizo.

Taratibu za kutupa maji taka

13.-(1) Mtu anayezalisha maji taka anawajibu kuwa na karo au kuhakikisha anayaelekeza katika mfumo wa maji taka au shimo rasmi lililoandaliwa kwa ajili ya

kusafirisha au kupokea au kuhifadhi maji taka.

(2) Wamiliki i wa viwanda wana wajibu wa kuelekeza maji taka ya viwandani katika mfumo rasmi wa kusafirisha maji taka au kuelekeza kwenye shimo au bwawa lililoandaliwa rasmi kwa ajili ya kutakasa au kuhifadhi maji ya viwanda.

Wajibu wa kudhibiti na kuondoa mazalia ya mbu na wadudu wengine

14. Kila mtu ana wajibu wa kudhibiti na kuondoa mazalia ya mbu na wadudu wengine.

Utaratibu wa kuchinja na kusafirisha nyama

15.-(1) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mfugo au mifugo mahali pengine popote ambapo si machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa na atalazimika kulipia gharama za machinjio kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Duka la nyama linatakiwa kuwa na-

(a) mwanga wa kutosha, kusakafiwa kwa marumaru nyeupe kwa urefu wa futi sita kutoka usawa wa ardhi;

(b) gogo la kukatia nyama au misumeno maalumu ya kukatia nyama;

(c) maji safi, meza, visu, mzani wa kawaida au wa kielektroniki na vyuma vya kuning'inizia nyama;

(d) wavu wa kuzuia inzi na wadudu wengine kwenye milango na madirisha; na

(e) pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini.

(3) Nyama inayouzwa itakaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na kugongwa muhuri na muuzaji atahakikisha kuwa nyama inauzwa ndani ya jengo

(4) Muuzaji atahakikisha anavaa sare maalum na anapima afya yake kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji;

(5) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalumu lililosajiliwa na kupewa cheti maalumu na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoidhinishwa na Halmashauri.

(6) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia kwenye machinjio au duka la nyama kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii ikibainika kuna jambo au mazingira yoyote ambayo ni hatarishi kwa afya ya binadamu ataamuru machinjio au bucha hilo kufungwa au kutekeleza maelekezo atakayoyatoa au kulipa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(7) Mmiliki wa bucha au Muuzaji wa nyama atalazimika kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wote wa ukaguzi.

Udhibiti na uzuiaji wa magonjwa ya mlipuko na tahadhari ya moto

16.-(1) Mtu anatakiwa kuchukua tahadhari zinazokubalika kwa mujibu wa Sheria za nchi ili kuzuia kutokea kwa magonjwa yote ya kuambukiza au yasiyoambukiza na kuchukua tahadhari dhidi ya moto kwa kuweka vifaa vya tahadhari ya moto katika eneo lake ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri.

(2) Mtu au taasisi au uongozi wa eneo lolote lenye mkusanyiko wa watu atawajibika kukubali kupatiwa chanjo ya kuzuia au kutibu ugonjwa wowote kama itakavyoelekezwa na Wizara ya Afya katika nyakati tofauti.

Usafi na utengenezaji wa vyakula,

17.-(1) Mtu au mmiliki wa maduka, hoteli au migahawa atakayetengeneza au kuonesha kwa kuuza

maji na vinywaji vingine

chakula au kutangaza ili kufanya biashara ya kuuza chakula mahali popote, mtaani, kichochoroni au katika nyumba yoyote atalazimika kupata kibali na usajili kutoka kwa Halmashauri kupitia kwa Afisa Mwidhiniwa.

(2) Mtu hataruhusiwa kuuza au kutangaza vyakula au vinywaji katika eneo la wazi lisilojengwa na vifaa vya kudumu isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka Halmashauri.

(3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuzuia upishi au utengenezaji wa pombe na vyakula katika mazingira yasiyoridhisha kiafya.

(4) Kila mfanyabiashara wa bidhaa za mboga mboga na matunda atalazimika kuuza bidhaa hizo juu ya kichanja.

Unyunyiziaji na upuliziaji wa viuatilifu

18. Mtu anayeendesha biashara ya unyunyiziaji au upuliziaji wa viuatilifu vya kuua wanyama au wadudu waharibifu atalazimika kupata kibali cha Halmashauri.

Usalama wa afya na tahadhari katika viwanda, nyumba na maeneo ya wazi

19.-(1) Mtu, taasisi au kampuni inayozalisha au kwa asili ya kazi wanazozifanya zinawapelekea kuzalisha uchafu, takataka, vumbi ama kitu kingine kama hicho chenye madhara kwa afya ya binadamu au viumbe wengine atalazimika kuandaa utaratibu wa kuhifadhi taka hizo katika hali isiyoweza kudhuru afya ya binadamu na viumbe wengine.

(2) Mtu ambaye ni msimamizi wa familia au biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa nyumba au mahali anapoishi au kufanya biashara panakuwa safi na salama kwa maisha ya binadamu.

Upandaji na utunzaji wa miti

20.-(1) Bila kuathiri matakwa ya kijiografia na kitaalamu ya upandaji na ukuzaji wa mazao mengine kila mmiliki wa ardhi katika eneo la Halmashauri atapanda angalau miti mitano katika eneo la kiwanja cha kawaida

cha makazi na kupanda angalau miti kumi kila mwaka kwa mashamba yenye ukubwa wa kuanzia hekari tatu.

(2) Mkazi wa Halmashauri atakuwa wajibu wa kushiriki katika zoezi la pamoja la upandaji miti litakaloandaliwa na Halmashauri kwa mujibu wa ratiba iliyowekwa.

(3) Mtu anayetaka kuvuna mti au miti katika eneo lolote ndani ya Halmashauri atalazimika kupata kibali kutoka Halmashauri kwa kulipia ada ya kibali.

Utunzaji wa vyanzo vya maji

21.-(1) Serikali ya Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata itabainisha na kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji vyanzo vyote vya maji vinavyopatikana katika eneo lao ikiwa ni pamoja na kuleta mapendekezo yaliyopitishwa na wananchi kupitia Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, kuhusu namna ya kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji katika maeneo yao.

(2) Kila mtu atatunza vyanzo vya maji vilivyoko katika Kijiji au Kitongoji anachoishi ikiwa ni pamoja na kushiriki zoezi la kufanya usafi na kupanda miti kwenye vyanzo vya maji kulingana na ratiba itakayowekwa.

(3) Mtu yeyote anayetaka kujenga nyumba au kufanya shughuli yoyote ya kiuchumi atalazimika kupata cheti maalumu kutoka Halmashauri kitakacho thibitisha kwamba jengo linalojengwa au mradi haupo ndani ya Mita Sitini kutoka kwenye chanzo cha maji na kwamba mradi husika hautakuwa na athari kwenye vyanzo vya maji.

Ukaguzi wa mazingira

22. Mtu yeyote anayeendesha mradi au anayekusudia kuanzisha mradi mdogo au mkubwa au kufanya ujenzi wa jengo lolote la kutolea huduma kama shule, hoteli, kanisa au kiwanda atalazimika kufanyiwa ukaguzi wa mazingira na kupata cheti kutoka Halmashauri na kulipa ada ya ukaguzi kama

ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Wajibu wa kushiriki usafi wa pamoja kila mwezi

23. Kila mtu atakuwa na wajibu wa kushiriki zoezi la usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi katika maeneo yatakayokuwa yamepangwa na kwa muda uliopangwa.

Utunzaji wa maeneo yasiyotumika

24.-(1) Kila mmiliki wa jengo, kontena, gari, kiwanja, shamba na kitu kingine chochote kilichopo kwenye mazingira atawajibika kukitunza kwa kufanya usafi na kukiweka katika hali ambayo hakiwezi kusababisha kero kwa watu au kufanyika makazi ya viumbe wanaoweza kumuathiri mtu au kiumbe chochote au kuwa maficho ya wahalifu au sehemu ya kutupia taka.

(2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kutunza jengo, eneo au kitu kingine chochote kilichotelekezwa ambacho mmiliki wake hajulikani na ambacho kinaleta kero katika mazingira na kitatangazwa katika maeneo ya wazi na kwenye vyombo vya habari kwa muda wa siku tisini, endapo mmiliki huyo hatajitokeza Halmashauri itafanya utaratibu wa kutwaa, na endapo mmiliki atajitokeza baadaye au wakati utaratibu wa kutwaa eneo au kitu hicho unafanyika atalazimika kulipa faini na gharama zote zilizotumika kusafisha na kutunza eneo, jengo au kitu hicho.

Utaratibu wa ufugaji

25.-(1) Mtu anayefanya shughuli za ufugaji katika kata zote zilizopo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo Ngaramtoni na maeneo ya miji atalazimika kufanya ufugaji wa ndani.

(2) Mtu anayekusudia kuanzisha mradi wa ufugaji atalazimika kuwa na cheti cha ukaguzi wa mazingira cha Halmashauri.

(3) Halmashauri itakamata mfugo au mifugo yoyote itakayoonekana inazurura hovyo katika eneo la

Halmashauri.

(4) Mfugo utakaokamatwa chini ya aya ndogo ya (3) utalipiwa faini ya Shilingi elfu kumi kwa kila siku.

(5) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(6) Bila kuathiri aya ndogo ya (5), Halmashauri kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada itamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(7) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo kutokana na sababu yoyote ile, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri

Udhibiti wa sauti na mitetemo

26.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kufanya matangazo au mkutano au tamasha au mkusanyiko wowote wa nje atahakikisha anapata kibali kutoka kwa Halmashauri.

(2) Kumbi zote za muziki au baa au kilabu au nyumba za ibada zenye kufanya mikesha zitalazimika kuweka sauti isiyoleta kero kwa majirani au kuwa na vifaa maalumu vya kuzuia sauti kutoka nje

Udhibiti wa uchafuzi wa hewa

27.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma taka isipokuwa kwa taka hatarishi zinazoruhusiwa kuteketezwa kwa utaratibu na kanuni maalumu.

(2) Mtu yeyote anayezalisha taka hatarishi atalazimika kuwa na kichomea taka kilichoandaliwa kitaalamu kwa ajili ya kuchomea taka hizo.

(3) Mtu yeyote mwenye kiwanda, shamba au mradi wowote unaotumia au kuzalisha kemikali hataweka kiwanda, shamba au mradi huo katika eneo la makazi na atalazimika kuwa na cheti cha ukaguzi wa mazingira kwa mujibu Sheria Ndogo hii.

Usalama katika mazingira ya migodi na ukaguzi

28.-(1) Mtu yeyote anaemiliki mgodi uliorasmi na usio rasmi ndani ya eneo la Halmashauri atalazimika kusajiliwa na kutambuliwa na Halmashauri ndani ya siku tisini tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria Ndogo hii, na atawajibika kulipa ada ya urejeshaji mazingira

(2) Migodi yote rasmi na isiyo rasmi itapaswa kukaguliwa na kupata cheti cha ukaguzi wa mazingira kutoka Halmashari.

(3) Mgodi wowote usio rasmi uliokaguliwa na kupatiwa cheti na Halmashauri utalazimika kufuata utaratibu wa kurasimisha machimbo hayo na kupata leseni ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kukaguliwa na kupewa cheti cha Halmashauri, na yeyote atakayeshindwa kutimiza masharti hayo atafungiwa mgodi na kulipa faini ya shilingi laki tatu.

(4) Afisa Mtendaji wa Kijiji atakuwa na wajibu wa kuorodhesha migodi yote iliyopo katika eneo lake na kuwasilisha kwa Mkurugenzi.

(5) Mtu yeyote anayetaka kuanzisha mgodi mpya atalazimika kupata kibali pamoja na cheti cha ukaguzi wa Mazingira cha Halmashauri sambamba na kufuata taratibu zote za kisheria za kuanzisha na kimiliki migodi.

(6) Kwa madhumuni ya aya hii “mgodi” unamaanisha machimbo ya aina yoyote ya madini ikiwemo udongo, moramu, kokoto na vifusi.

Shughuli za kilimo

29.-(1) Mtu anayefanya shughuli za kilimo ndani ya Halmashauri atalazimika kuzingatia kilimo rafiki kwa mazingira.

(2) Mtu anayeandaa shamba kwa kuchoma moto atalazimika kupata kibali cha Halmashauri.

(3) Mtu anayelima kwenye mteremko analazimika kuzingatia kanuni za kilimo kwenye miteremko au miinuko.

(4) Mtu anaelima karibu na vyanzo vya maji atalazimika kuwa nje ya mita sitini na atatunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti na mimea inayokubalika katika maeneo hayo.

(5) Mtu yeyote anayefanya mradi wa kilimo cha umwagiliaji atalazimika kupata kibali cha Halmashauri.

Shughuli za usafirishaji na utunzajia wa barabara

30.-(1) Mmiliki wa chombo cha usafiri atahakikisha kuwa chombo chake cha usafiri kinabeba mzigo wenye uzito unaokubalika katika barabara husika ili kuepusha uharibifu wa barabara za Halmashauri.

(2) Mtu atatakiwa kupitisha mifugo katika barabara rasmi zilizotengwa kwa ajili ya kupitisha mifugo tu.

(3) Mmiliki wa nyumba au kiwanja au mpangaji atahakikisha mtaro au kalavati ya kutiririsha maji ya mvua iliyo kando ya barabara mbele ya nyumba yake inakuwa safi muda wote.

Maeneo ya kuoshea magari

31. Mtu anayekusudia kuanzisha biashara ya kuosha magari atalazimika kuomba kibali kutoka Halmashauri, na ukaguzi wa mazingira utafanyika na afisa mwidhiniwa akiridhika atampatia cheti cha ukaguzi wa mazingira baada ya kulipa ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Matangazo na mikutano

32. Mtu anayekusudia kufanya matangazo au mkutano wa hadhara atatakiwa kuomba kibali kwa Halmashauri na kulipa ada kama zilivyoanishwa katika Jedwali la Tatu.

Biashara ya kuupulizia na kuua wadudu

33. Mtu anayekusudia kuanzisha biashara ya kupulizia dawa ya kuuwa wadudu waenezao magonjwa kwa binadamu atalazimika kuomba kibali kutoka halmashauri, na ukaguzi wa mazingira utafanyika na afisa mwidhiniwa akiridhika atampatia cheti cha ukaguzi wa mazingira baada ya kulipa ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Uteuzi wa wakala

34.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa

35. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

(a) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atajisaidia haja kubwa au ndogo mahali ambapo sio chooni;

(c) hatajenga choo katika jengo au eneo lake;

(d) atachimba shimo la maji taka bila kibali cha Halmashauri;

(e) atasababisha shimo la maji taka au bwawa la maji taka au chemba ya choo kupasuka au kuziba kwa bomba la maji taka na kutiririsha

maji taka;

(f) atatupa taka katika eneo ambalo halikutengwa kwa ajili ya kutupia taka;

(g) atasafirisha taka bila kuzifunika;

(h) atatupa taka hatarishi katika mazingira yoyote bila kuchukuwa tahadhari au kufuata taratibu;

(i) atakusanya ushuru wa taka bila kibali cha Halmashauri au kuchelewa kulipa ada ya taka kwa muda ulioainishwa;

(j) atatiririsha au kumwaga maji taka barabarani, uchochoroni, kwenye mifereji, mtoni, kwenye vyanzo vya maji au sehemu nyingine yoyote isiyotengwa kwa ajili ya kuhifadhia au kusafirisha maji taka;

(k) atatupa kemikali yabisi, kimiminika au kemikali za gesi katika maeneo yasiyo rasmi;

(l) atahifadhi au kuweka viuatilifu kwenye chumba au ghala au stoo au eneo linalofanana na hilo bila idhini ya Halmashauri;

(m) ataruhusu mazalia ya mbu au wadudu wengine;

(n) atatelekeza eneo au kitu chochote anachomiliki kiasi cha kuleta kero au kusababisha madhara kwa wengine;

(o) ataanzisha au kuendesha biashara ya kuosha magari bila kibali cha Halmashauri;

(p) ataelekeza mtaro wa maji ya mvua au maji taka au kutupa takataka barabarani;

(q) atasafirisha mzigo uliozidi uzito, au kupitisha mfugo au mifugo au kuelekeza maji machafu au kutupa takataka barabarani;

(r) ataacha mitaro ya maji ya mvua iliyopo mbele ya nyumba kuwa michafu;

(s) atafanya shughuli za kilimo kinyume na shughuli za Sheria Ndogo hii;

(t) atamiliki au kuanzisha mradi wa kufuga nguruwe bila ya kuwa na cheti cha ukaguzi wa mazingira;
(u) ataizurulisha au kupitishwa katika barabara za Halmashauri ambazo si rasmi kwa ajili ya mifugo;
(v) atauza au kutaka kuuza kwenye halaiki ama hadharani kwenye kundi la watu ama kwa mtu mmoja pombe, maji ama chakula bila kupata idhini ya Halmashauri;
(w) atauza mboga mboga au matunda kwa kuweka ardhini; na
(x) atauza au kutumia au kutoa kama msaada kwa mtu bidhaa yoyote ambayo imekwisha muda wa matumizi;
(y) ataweka nembo yoyote juu ya kifungashio cha bidhaa ya chakula ambayo haina uhalisia wa kile kilichopo ndani;
(z) atauza vipodozi vyenye viambata sumu kwa mujibu wa Sheria na kanuni zinazo simamia uuzaji na utengeneza jiwa vipodozi;
(aa) atakata mti bila kibali, au kuacha eneo la ardhi analolimiliki bila kupanda miti, au atakayekaidi kushiriki zoezi la pamoja la upandaji miti;
(bb) atajenga ndani ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji, kufanya shughuli yoyote ya kiuchumi inayoharibu chanzo, kuelekeza maji taka ya nyumbani au viwandani au kufua nguo, kuosha vyombo au kuoga kwenye chanzo cha maji;
(cc) ataanzisha mgodi kwenye eneo la makazi ya watu, kando kando ya miundombinu ya barabara, shule na maeneo mengine ya huduma za jamii, au kuchimba na kuacha

mashimo yanayohatarisha maisha ya watu katika mazingira; au

(dd) ataweka au kutaka kuweka kitu chochote chenye kutoa sauti au mitetemo inayoweza kuleta madhara ya kiafya au ambayo ni kero na kwa jamii inayozunguka eneo hilo.

Adhabu

36. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi elfu hamsini na kisichozidi Shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

37. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi cha Shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 12(1)*)

USHURU WA UZOAJI NA UTUPAJI TAKA NGUMU

| Namba. | Aina ya Jengo | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Duka la jumla | 10,000/= |
| 2. | Duka la rejareja au nafaka au Steshenari au stoo ya vinywaji | 5,000/= |
| 3. | Taka za nyumbani | 3,000/=- |
| 4. | Fundi au msafisha viatu | 2000/= |
| 5. | Kibanda cha matunda au genge | 2000/= |
| 6. | Bucha | 5000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Mama au Baba lishe | 5000/= |
| 8. | Mashine ya kusaga na kukoboa | 5000/= |
| 9. | Duka la dawa muhimu | 5000/= |
| 10. | Duka la vipuri | 5000/= |
| 11. | Saluni ya kiume au kike | 5000/= |
| 12. | Studio | 3000/= |
| 13. | Fundi cherehani | 5000/= |
| 14. | Gereji ya kuchomelea | 5000/= |
| 15. | Baa | 12000/= |
| 16. | Duka la vinywaji baridi na pombe | 10,000/= |
| 17. | Duka la vifaa vya ujenzi | 10,000/= |
| 18. | Karakana | 10,000/= |
| 19. | Gereji | 20,000/= |
| 20. | Mgahawa | 10,000/= |
| 21. | Sehemu ya kutengeneza matofali | 20000/= |
| 22. | Mashine ya kuchana mbao | 20000/= |
| 23. | Mini Supermarket | 10000/= |
| 24. | Kituo cha mafuta | 50000/= |
| 25. | Fundi seremala | 5000/= |
| 26. | Kiwanda kikubwa | 10,000/= |
| 27. | Kiwanda cha kati | 60,000/= |
| 28. | Kiwanda kidogo | 30,000/= |
| 29. | Hoteli kubwa | 100,000/= |
| 30. | Hoteli ya kati | 45,000/= |
| 31. | Nyumba ya kulala wageni | 25,000/= |
| 32. | Hospitali | 50,000/= |
| 33. | Kituo cha afya na Zahanati | 30,000/= |
| 34. | Ofisi | 30,000/= |
| 35. | Mkandarasi wa majengo | 50,000/= |
| 36. | Duka la vifaa vya magari | 15,000/= |
| 37. | Ofisi ya Wakili | 10,000/= |
| 38. | Ofisi ya mtaalamu wa kuuwa wadudu | 10,000/= |
| 39. | Ghala kubwa | 50,000/= |
| 40. | Ghala la kati | 30,000/= |
| 41. | Ghala dogo | 20,000/= |
| 42. | Ofisi ya Mhasibu au Mkaguzi na huduma za kompyuta | 20,000/= |
| 43. | Taka za bustani | 180,000/= kwa safari moja |
| 44. | Jumba la sinema | 20,000/= |
| 45. | karakana | 20,000/= |
| 46. | Ada ya kutupa taka kutoka kwenye mkokoteni ndani ya kizimba | 5,000.00/= |
| 47. | Huduma ya kufua na kunyoosha | 10,000.00/= |
| 48. | Uwanja wa maonesho | 10,000.00/= |
| 49. | Kiwanja cha michezo | 20,000.00/= |

| | | |
|---|---|---|
| 50. | Shule ya kutwa | 20,000.00/= |
| 51. | Kituo cha kutunza watoto | 10,000.00/= |
| 52. | Stendi kubwa ya Basi | 80,000.00/= |
| 53. | Stendi ndogo ya Basi | 40,000.00/= |
| 54. | Ukarabati wa vifaa vya umeme | 10,000.00/= |
| 55. | Kizimba cha soko | 300/= kwa siku |
| 56. | Kutupa taka kwenye dampo | 50,000/= kwa safari moja |
| 57. | Hoteli yenye baa au kumbi za starehe na sherehe | 200,000/= |
| 58. | Benki tawi kubwa | 100,000/= |
| 59. | Benki tawi dogo | 60,000/= |
| 60. | Mikutano ya hadhara au dini au semina au kongamano | 20,000/= kwa siku |
| 61. | Shule ya bweni | 50,000/= |
| 62. | Biashara yoyote ambayo haijaainishwa | 10,000/= |

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 12 na 22*)

ADA ZA UKAGUZI WA MAZINGIRA USAJILI NA VIBALI

| Namba. | Aina ya Shughuli | Ada ya Usajili. | Ada ya Ukaguzi wa Mazingira na Kibali kwa Mwaka. |
|---|---|---|---|
| 1. | Migodi ya madini ya ujenzi | 20,000/= | 50,000/= |
| 2. | Eneo la kuoshea magari | 10,000/= | 20,000/= |
| 3. | Minara ya simu | 20,000/= | 50,000/= |
| 4. | Ujenzi wa jengo hadi ghorofa moja. | | 50,000/= |
| 5. | Ujenzi wa ghorofa 2 hadi 5 | | 100,000/= |
| 6. | Ujenzi wa ghorofa 6 na kuendelea | | 300,000/= |
| 7. | Mradi wa kilimo | | 50,000/= |
| 8. | Kibali cha kupakua maji taka | | 50,000/= |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 32)*

| Namba. | Aina ya Kibali | | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| | Kibali cha kufanya Matangazo au Mikutano ya Hadhara | | 50,000/= kwa siku |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 33)*

VIWANGO VYA MALIPO YA UKAGUZI, USAJILI, KUPIMA AFYA NA KUPULIZIA DAWA YA KUUWA WADUDU WAENEZAO MAGONJWA KWA BINADAMU

| Namba. | AINA YA BIASHARA | UKAGUZI | KIPIMA AFYA | KUPILIZIA DAWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Maduka ya Rejareja. | 10,000 | 10,000 | Mtu au kampuni itakayoomba kibali cha kupulizia dawa italipa ada ya kibali Sh. 100,000/= |
| 2. | Bucha | 30,000 | 10,000 | |
| 3. | Nyumba za Wageni | 30,000 | 10,000 | |
| 4. | Maduka ya Jumla | 20,000 | 10,000 | |
| 5. | Migahawa | 10,000 | 10,000 | |
| 6. | Mashine ya Kusaga | 10,000 | 10,000 | |
| 7. | Mifigo/kilimo | 10,000 | 10,000 | |
| 8. | Hoteli | 100,000 | 10,000 | |
| 9. | Vipodozi | 10,000 | 10,000 | |
| 10. | Dawa za binadamu | 20,000 | 10,000 | |
| 11. | Chuo | 100,000 | 10,000 | |
| 12. | Stoo ya Vinywaji | 20,000 | 10,000 | |
| 13. | Garage | 20,000 | 10,000 | |
| 14. | Vifaa vya Ujenzi | 20,000 | 10,000 | |
| 15. | Mwafrika Bar | 10,000 | 10,000 | |
| 16. | Restaurant/on bar | 20,000 | 10,000 | |
| 17. | Maduka ya nafaka | 20,000 | 10,000 | |
| 18. | Stationary | 10,000 | 10,000 | |
| 19. | Spareparts | 20,000 | 10,000 | |
| 20. | kinyozi | 10,000 | 10,000 | |
| 21. | Saloon za kike | 10,000 | 10,000 | |
| 22. | Ghala/Godown | 50,000 | 10,000 | |
| 23. | Viwanda | 100,000 | 10,000 | |
| 24. | Shule za Binafsi zenye wanafunzi zaidi ya 700 | 100,000 | 10,000 | |
| 25. | Shule Binafsi zenye wanafunzi wasiozidi 700 | 70,000 | 10,000 | |
| 26. | Timberyard/sawmil | 50,000 | 10,000 | |
| 27. | Matofali | 50,000 | 10,000 | |
| 28. | Petrostation | 100,000 | 10,000 | |
| 29. | Karakana | 20,000 | 10,000 | |
| 30. | Minisupermarket | 20,000 | 10,000 | |
| 31. | Shamba la Maua | 100,000 | 10,000 | |
| 32. | Pub/grocery | 20,000 | 10,000 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 33. | Wachoma nyama | 10,000 | 10,000 | |
| 35. | Fundi cherehani | 10,000 | 10,000 | |
| 36. | Bustani za maua | 10,000 | 10,000 | |
| 37. | Viwanda vya ushonaji | 20,000 | 10,000 | |
| 38. | Machimbo ya mawe/moram na madini mengine. | 100,000 | 10,000 | |
| 39. | Day care | 20,000 | 10,000 | |
| 40. | Safari &campsite | 100,000 | 10,000 | |
| 41. | Kambi za muda | 50,000 | 10,000 | |
| 42. | bakery | 20,000 | 10,000 | |
| 43. | Magari ya kubeba vyakula | 30,000 | 10,000 | |
| 44. | Depot | 100,000 | 10,000 | |

## JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 37)*

### FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya aya ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ....................................................

MBELE YA:
Jina……...............................................
Wadhifa: .............................................
Saini: ....................................................
Tarehe: ..............................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Arusha imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamoTarehe 10 mwezi Mei 2023 mbele ya:-

SELEMAN HAMISI MSUMI
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Arusha*

OJUNG'U SALEKWA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Arusha*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*